Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum

MWONGOZO WA URATIBU WA PROGRAMU JUMUISHI YA TAIFA YA MALEZI MAKUZI NA MAENDELEO YA AWALI YA MTOTO (PJT-MMMAM) 2021/22–2025/26

DESEMBA, 2023

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake
na Makundi Maalum

MWONGOZO WA URATIBU WA PROGRAMU JUMUISHI YA TAIFA YA MALEZI MAKUZI NA MAENDELEO YA AWALI YA MTOTO (PJT-MMMAM) 2021/22–2025/26

Desemba, 2023

YALIYOMO

VIFUPISHO.....vi
FASILI YA MANENO.....vii
DIBAJI.....viii

1.0 UTANGULIZI.....1
1.1 Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM).....1
1.2 Malengo ya Mwongozo.....2
1.2.1 Malengo Mahsusi.....2
1.3 Walengwa wa Mwongozo.....2
1.4 Mifumo ya utekelezaji wa PJT-MMMAM.....2
1.5 Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu, Miongozo ya Kitaifa, Mikataba ya Kikanda na Kimataifa.....3
1.6 Uzingatiaji wa Masuala Mtambuka katika PJT-MMMAM.....3

2.0 MUUNDO WA URATIBU WA PJT-MMMAM.....3
2.1 Ngazi ya Taifa.....4
2.1.1 Wizara yenye dhamana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.....4
2.1.2 Ofisi ya Waziri Mkuu.....4
2.1.2.1 Kikao cha Mawaziri.....5
2.1.2.2 Kikao cha Makatibu Wakuu.....6
Majukumu ya Kikao cha Makatibu Wakuu.....6
2.1.2.3 Kikao cha Kamati Tendaji ya PJT-MMMAM.....7
2.1.3 Wizara yenye dhamana na Mtoto.....9
Majukumu ya Wizara yenye dhamana na Mtoto.....9
2.1.3.1 Sekretarieti ya PJT-MMMAM Ngazi ya Taifa.....10
2.1.4 Wizara yenye dhamana na Afya.....12
2.1.5 Wizara yenye dhamana na Elimu.....13
2.1.6 Wizara yenye dhamana na Mambo ya Ndani ya Nchi.....13
2.1.7 Wizara yenye dhamana na Fedha.....14
2.1.8 Wizara yenye dhamana na Watu wenye Ulemavu.....14

2.1.9 Ngazi ya Mkoa.....15
2.1.10 Ngazi ya Wilaya.....16
2.1.11 Ngazi ya Kata 17
Uratibu wa PJT-MMMAM ngazi ya Kata.....17
2.1.12 Ngazi ya Kijiji/Mtaa.....18
Uratibu wa PJT-MMMAM ngazi ya Kijiji/Mtaa.....18

3.0 UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA PJT- MMMAM.....19
3.1 Ufuatiliaji na tathmini.....19
3.2 Utoaji Taarifa ya Utekelezaji wa PJT-MMMAM.....20

4.0 HITIMISHO.....21

VIFUPISHO

MMMAM	Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto
MTAKUWWA	Mpango Kazi wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto
OR - TAMISEMI	Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
OWM-(SBU)	Ofisi ya Waziri Mkuu (Sera, Bunge na Uratibu)
PJT-MMMAM	Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto
UKIMWI	Upungufu wa Kinga wa Mwilini
WMJJWM	Wizara ya Maendelo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum

FASILI YA MANENO

Afua: Ni shughuli au kazi mbalimbali zilizobainishwa katika Mwongozo.

Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (MMMAM): Kwa muktadha huu ni hatua jumuishi zenye muunganiko wa vipengele vyote vya MMMAM katika ukuaji wa mwili, akili, lugha, kijamii, kitamaduni, kihisia na kimaadili**.**

Mtoto mwenye ulemavu: Ni Mtoto ambaye ana tatizo la kimwili, kiakili, au kihisia ambalo linazuia au kupunguza ushiriki wake katika mambo ya kijamii akilinganishwa na watoto wengine wasio na ulemavu.

Wadau: Ni Taasisi/Mashirika au mtu binafsi anayeshiriki katika utekelezaji wa miradi au programu za maendeleo. Hii inahusisha Mashirika ya Umoja wa Mataifa, Mashirika Wafadhili na ya Kimataifa, Asasi za Kiraia, Mashirika ya Dini,Sekta Binafsi na Jamii.

Sekretariati ya utekelezaji wa PJT-MMMAM: Ni kikosi cha uratibu wa utekelezaji wa shughuli zote za PJT-MMMAM ngazi ya Taifa.

Wasimamizi wa MMMAM- Ni wataalam wa masuala ya MMMAM katika Sekta ya Afya, Elimu, Lishe na Maendeleo ya Jamii katika Sekretarieti ya Mikoa na Mamalaka za Serikali za Mitaa.

DIBAJI

Serikali kwa kushirikiana na Wadau wa watoto imeandaa Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM) itakayo tekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano (2021/22-2025/26). Programu hii inalenga kutatua changamoto na kuboresha upatikanaji wa huduma za malezi jumuishi yenye vipengele vitano: 1. Afya bora kwa mtoto na mama/mlezi; 2. Lishe ya kutosha kuanzia ujauzito; 3. Malezi yenye mwitikio; 4. Fursa za ujifunzaji wa awali; na 5. Ulinzi na usalama wa mtoto.

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais -TAMISEMI pamoja na Wizara za Kisekta na Wadau chini ya uratibu wa Ofisi ya Waziri Mkuu- (Sera, Bunge na Uratibu) imeandaa Mwongozo wa Uratibu wa PJT-MMMAM ili kuboresha utekelezaji wa afua mbalimbali zilizoainishwa katika programu hiyo. Lengo ni kusaidia utekelezaji, usimamizi, ufuatiliaji na utoaji taarifa za maendeleo ya shughuli za MMMAM katika ngazi ya Taifa, Mkoa, Halmashauri na Jamii. Ni imani yetu kwamba, kupitia Mwongozo huu matokeo ya haraka na chanya ya maendeleo ya awali ya mtoto yatapatikana kwa kuwepo uratibu na ushiriki wa sekta mbalimbali katika kutoa huduma za malezi jumuishi.

Afua zote zinapaswa kutekelezwa kwa ujumuishi kwa kuwa zinalenga kuleta matokeo chanya katika ukuaji na maendeleo ya awali ya mtoto na kufikia maono ya programu hii: "*Watoto wote Tanzania wapo kwenye mwelekeo sahihi wa kufikia ukuaji timilifu*". Mwongozo huu utaunganisha juhudi na rasilimali za wadau wote katika kutekeleza afua zilizopangwa katika PJT - MMMAM ili kuleta ufanisi wa hali ya juu na kufikia malengo ya programu.

Natoa wito kwa wadau kushiriki kufanikisha maono ya programu hii kwa kuhakikisha wanajielekeza kuchangia utekelezaji kwa kufanya kazi kwa karibu na Serikali kupitia muundo na taratibu zilizoainishwa katika Muongozo huu. Aidha, upatikanaji wa rasilimali za kutosha ikiwemo rasilimali fedha na rasilimali watu ni suala la muhimu katika kufanikisha utekelezaji wa programu hii. Kupitia jitihada jumuishi zinazoratibiwa kwa ufanisi, kwa pamoja tutahakikisha Watoto wote wa Tanzania wanaishi na kustawi.

Dkt. Seif Abdallah Shekalaghe

KATIBU MKUU

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum

1.0 UTANGULIZI

1.1 Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM)

Mnamo Desemba, 2021 Serikali ilizindua Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM). Programu hiyo inalenga kuharakisha upatikanaji wa matokeo chanya ya maendeleo ya awali ya mtoto kwa kuboresha mfumo shirikishi wa kisekta katika malezi na makuzi ya mtoto yakijumuisha upatakinaji wa huduma bora za Afya, Lishe, Malezi yenye mwitikio, Fursa za Ujifunzaji wa Awali na Ulinzi na Usalama. Programu inatekelezwa kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia 2021/22 hadi 2025/26 inasaidia utekelezaji wa mifumo ya uratibu kwa kuleta pamoja sheria na sera mbalimbali zinazohusiana na malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto, ikiwemo Sheria ya Mtoto Sura ya 13, Sera ya Maendeleo ya Mtoto ya (2008) Sera ya Elimu na Mafunzo (2014),Sera ya Taifa ya Maendeleo na Huduma kwa Watu Wenye Ulemavu (2004) na Sera ya Afya (2007) kwa lengo la kushughulikia mahitaji jumuishi ya maendeleo ya mtoto (miaka 0-8).

Programu hii inalenga kuimarisha ushirikiano baina ya Serikali na wadau ili kuhakikisha Watoto wote nchini Tanzania wanapata huduma za Malezi jumuishi ili kufikia ukuaji timilifu. Aidha, Programu inatambua uwepo wa Programu nyingine za kitaifa ambazo zinatumia mifumo shirikishi wa Kisekta katika maendeleo ya Mtoto ikijumuisha Programu Jumuishi ya Taifa ya Lishe (NMNAP II – 2021/22-2025/26) na Mpango wa Taifa wa Kutokomeza Ukatili Dhidi ya Wanawake na Watoto (MTAKUWWA 2017/18-2021/22). PJT-MMMAM itachangia programu za kitaifa zilizopo kwa kutumia fursa zilizoainishwa na kushughulikia mapungufu yaliyopo ili kuboresha utoaji wa huduma jumuishi za malezi, makuzi na maendeleo ya awali ya watoto wote nchini.

1.2 Malengo ya Mwongozo

1.2.1 Lengo Kuu

Mwongozo wa PJT-MMMAM unalenga kuimarisha uratibu katika ngazi zote za utekelezaji wa Programu. Aidha, Mwongozo unaelezea majukwaa na vikao mbalimbali vyenye lengo la kufuatilia, kutathmini na kushauri juu ya utekelezaji wa PJT-MMMAM kwenye ngazi zote.

1.2.2 Malengo Mahsusi

1. Kuimarisha mifumo ya uratibu na usimamizi wa PJT-MMMAM kuanzia ngazi ya Taifa, Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;
2. Kuimarisha mifumo ya ufuatiliaji, tathmini na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa PJT-MMMAM.

1.3 Walengwa wa Mwongozo

Walengwa wa mwongozo huu ni Wizara mbalimbali, Idara na Taasisi za Serikali, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na wadau wakiwemo Taasisi za Elimu, Taasisi za dini, Mashirika ya Kimataifa, Asasi za Kiraia, Vyombo vya Habari, Sekta binafsi na Jamii kwa ujumla. Hivyo, ushirikiano kati ya Serikali na wadau ni muhimu katika kufikia malengo ya utekelezaji wa PJT-MMMAM.

1.4 Mifumo ya utekelezaji wa PJT-MMMAM

Programu itatekelezwa kwa kuzingatia mifumo mbalimbali inayoshughulikia masuala ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto katika ngazi ya Taifa, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Mifumo hiyo inajumuisha vikao vya kisheria na kamati mbalimbali ikiwa ni pamoja na Kamati za Usalama, Kamati za ushauri, Kamati za Ulinzi na Usalama wa Mwanamke na Mtoto, kamati za Watu Wenye Ulemavu, Kamati za Lishe, Kamati za UKIMWI na Kamati za Afya.

1.5 Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu, Miongozo ya Kitaifa, Mikataba ya Kikanda na Kimataifa

Uratibu wa PJT-MMMAM unazingatia Sera, Sheria, Kanuni, Taratibu, Miongozo ya Kitaifa pamoja na Mikataba ya Kikanda na Kimataifa iliyorasimishwa nchini.

1.6 Uzingatiaji wa Masuala Mtambuka katika PJT-MMMAM

Mifumo ya uratibu katika ngazi zote za utekelezaji wa PJT-MMMAM izingatie masuala mtambuka ikiwa pamoja na uwiano wa kijinsia na ujumuishwaji wa watoto wenye mahitaji maalum katika jamii. Hivyo, mifumo hiyo ihakikishe kuwa huduma zote za MMMAM zinazingatia masuala mtambuka.

2.0 MUUNDO WA URATIBU WA PJT-MMMAM

Uratibu wa programu hii upo katika ngazi mbalimbali ambapo, kwenye ngazi ya Taifa, uratibu katika uongozi wa Programu utakuwa chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Bunge na Uratibu (OWM-SBU). Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (OR-TAMISEMI) itaratibu na kusimamia utekelezaji wa PJT-MMMAM katika Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa. Aidha, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum (WMJJWM) yenye dhamana ya kusimamia masuala ya watoto inaratibu utekelezaji wa PJT-MMMAM katika ngazi ya Taifa.

PJT-MMMAM inaratibiwa kupitia mifumo iliyopo kuanzia ngazi ya Taifa, Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kufikia malengo yaliyowekwa kama ifuatavyo:

2.1 Ngazi ya Taifa

2.1.1 Wizara yenye dhamana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

Wizara yenye dhamana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itahusika na kuratibu na kusimamia utekelezaji wa vipengele vya MMMAM kwa kuzingatia Sera, Mikakati, Kanuni na Miongozo ya Wizara za Kisekta na kutenga rasilimali kwa ajili kutekeleza afua mahususi za MMMAM katika Tawala za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

Majukumu ya Wizara yenye dhamana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

a) Kuratibu utekelezaji wa PJT-MMMAM kwenye Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ikiwemo utengaji wa fedha

b) Kupokea, kuchambua na kuandaa taarifa za Utekelezaji wa Programu kutoka kwenye Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na kuwasilisha katika Sekretarieti ya Taifa ya MMMAM.

2.1.2 Ofisi ya Waziri Mkuu.

Ofisi ya Waziri Mkuu – Sera, Bunge na Uratibu (OWM - SBU) itakuwa na majukumu yafuatayo:

i. Kuratibu na kuongoza vikao vya Mawaziri wa Wizara zinazohusika na utekelezaji wa PJT-MMMAM. Kikao cha Mawaziri kitakuwa na jukumu la kupokea taarifa ya utekelezaji wa programu kutoka kwa Makatibu Wakuu wa Wizara zinazohusika na utekelezaji wa PJT-MMMAM. Kikao hicho kitafanyika mara mbili kwa mwaka.

ii. Kuratibu na kuongoza vikao vya Makatibu Wakuu wa Wizara zinazohusika na utekelezaji wa PJT-MMMAM. Kikao cha Makatibu Wakuu kitapokea na kujadili taarifa ya utekelezaji wa PJT-MMMAM kutoka kwa wakurugenzi wa Wizara zinazohusika na utekelezaji wa PJT-MMMAM. Kikao hicho kitafanyika mara mbili kwa mwaka.

iii. Kuratibu kikao cha kamati tendaji ya Wakurugenzi wa Wizara, Wakala na Taasisi za Serikali na zisizo za Serikali zinazohusika na utekelezaji wa PJT-MMMAM. Kikao hicho kitafanyika kila robo mwaka.

iv. Kuhakikisha vikao vilivyoainishwa vinafanyika.

2.1.2.1 Kikao cha Mawaziri

Majukumu ya Kikao cha Mawaziri

i. Kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji zilizowasilishwa na Kikao cha Makatibu Wakuu

ii. Kutoa maelekezo ya kisera kuhusu taarifa iliyowasilishwa

Wajumbe wa kikao cha Mawaziri wa Wizara zinazohusika na utekelezaji wa PJT-MMMAM

i. Waziri mwenye dhamana na uratibu wa shughuli za Serikali (Mwenyekiti)
ii. Waziri mwenye dhamana na watoto
iii. Waziri mwenye dhamana na watu wenye ulemavu
iv. Waziri mwenye dhamana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa
v. Waziri mwenye dhamana na Afya
vi. Waziri mwenye dhamana na Mambo ya Ndani ya Nchi
vii. Waziri mwenye dhamana na Elimu
viii. Waziri mwenye dhamana na Fedha
ix. Waziri mwenye dhamana na Mipango

Waziri mwenye dhamana na uratibu wa shughuli za Serikali anaweza kuwaalika wajumbe wengine ambao hawajatajwa katika mwongozo huu kadri atakavyoona inafaa

2.2.1.2 Kikao cha Makatibu Wakuu

Majukumu ya Kikao cha Makatibu Wakuu

i. Kupokea na kujadili taarifa za utekelezaji zilizowasilishwa na Kikao cha Kamati Tendaji

ii. Kuridhia na kuwasilisha taarifa iliyojadiliwa kwenye Kikao cha Mawaziri

Wajumbe wa kikao cha Makatibu Wakuu wa Wizara zinazohusika na utekelezaji wa PJT-MMMAM

i. Katibu Mkuu mwenye dhamana na uratibu wa shughuli za Serikali (Mwenyekiti)

ii. Katibu Mkuu mwenye dhamana na watoto

iii. Katibu Mkuu mwenye dhamana na watu wenye ulemavu

iv. Katibu Mkuu mwenye dhamana na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa

v. Katibu Mkuu mwenye dhamana na Afya

vi. Katibu Mkuu mwenye dhamana na Mambo ya Ndani ya Nchi

vii. Katibu Mkuu mwenye dhamana na Elimu

viii. Katibu Mkuu mwenye dhamana na Fedha

ix. Katibu Mkuu mwenye dhamana na Mipango

x. Katibu Mkuu mwenye dhamana na uratibu wa shughuli za Serikali anaweza kuwaalika wajumbe wengine ambao hawajatajwa katika mwongozo huu kadri atakavyoona inafaa

2.2.1.5 Kikao cha Kamati Tendaji ya PJT-MMMAM:

Majukumu ya Kamati Tendaji

i. Kupitia taarifa za utekelezaji wa PJT-MMMAM za kila robo mwaka zilizowasilishwa na Sekretarieti

ii. Kupokea na kuridhia taarifa ya utekelezaji ya PJT-MMMAM kwa ajili ya kuwasilisha katika Kikao cha Makatibu Wakuu

Wajumbe wa kikao cha Kamati Tendaji ya PJT-MMMAM:

i. Mkurugenzi wa Sera na uratibu wa shughuli za Serikali – OWM (Mwenyekiti)

ii. Mkurugenzi wa Maendeleo ya Mtoto – WMJJWM (Makamu Mwenyekiti)

iii. Mkurugenzi Serikali za Mitaa - OR TAMISEMI

iv. Mkurugenzi Kitengo cha Watu wenye ulemavu- OWM-KVAU

v. Mkurugenzi Msaidizi Elimu ya Awali na Msingi - OR TAMISEMI

vi. Mkurugenzi wa Afya, Ustawi wa Jamii na Lishe OR - TAMISEMI

vii. Mkurugenzi wa Sera na Mipango - WMJJWM

viii. Kamishna Ustawi wa Jamii - WMJJWM

ix. Mkurugenzi Idara ya Mama na Mtoto - Wizara ya Afya

x. Kamishna wa Elimu - Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

xi. Mkurugenzi wa Uthibiti Ubora - Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

xii. Kamishna wa Bajeti – Wizara ya Fedha

xiii. Mkuu wa dawati la jinsia na Watoto Jeshi la Polisi Taifa

xiv. Mkuu wa Polisi Jamii

xv. Mkurugenzi Wizara ya Mambo ya Ndani anayehusika na masuala ya Watoto

xvi. Mkurugenzi Mtendaji wa TECDEN

xvii. Uwakilishi wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa yanayojishughulisha na masuala ya watoto;

xviii. Uwakilishi wa mashirika ya kimataifa yanayojishughulisha na masuala ya watoto;

xix. Uwakilishi wa Sekta Binafsi

xx. Uwakilishi wa watu wenye ulemavu

xxi. Uwakilishi wa Taasisi za Dini.

Vikao vya kamati tendaji ya PJT-MMMAM;

- Kikao cha Kitaifa cha Wataalam wa PJT-MMMAM kitafanyika kila robo mwaka na kutakuwa na vikao vya dharura pale inapohitajika.
- Akidi ya wajumbe wa kikao cha Kitaifa cha Wataalam wa PJT-MMMAM itakuwa zaidi ya nusu ya wajumbe akiwemo mwenyekiti .

2.1.3 Wizara yenye dhamana na Mtoto

Wizara yenye dhamana na mtoto itaratibu na kusimamia utekelezaji wa shughuli zote za PJT-MMMAM ngazi ya Taifa. Pia itahakikisha malengo yote ya programu yanafikiwa kama yalivyopangwa.

Majukumu ya Wizara yenye dhamana na Mtoto

Wizara itaratibu ujumuishwaji wa masuala ya MMMAM katika Sera, Mikakati, Programu, Kanuni na Miongozo; na kuratibu upatikanaji wa rasilimali za utekelezaji wa PJT-MMMAM. Majukumu mengine ni pamoja na:

a) Kuratibu na kuongoza vikao vya sekretarieti ya PJT-MMMAM.

b) Makamu Mwenyekiti wa vikao vya Mawaziri, Makatibu Wakuu pamoja na Kamati Tendaji ya PJT-MMMAM

c) Kujenga uelewa wa Wizara za kisekta kuhusu PJT-MMMAM

d) Kutoa maelekezo ya Utekelezaji wa Programu kwa Ngazi za Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kupitia OR-TAMISEMI

e) Kusimamia vigezo vya ubora wa utoaji huduma za PJT-MMMAM

f) Kushirikiana na Wadau katika utekelezaji wa PJT-MMMAM

g) Kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa PJT-MMMAM kwenye vikao vya uratibu ngazi ya Taifa

h) Kuratibu mkutano wa jukwaa la wadau unaofanyika kila baada ya miaka miwili. Aidha, Washiriki wa Jukwaa la Wadau wa PJT-MMMAM watakuwa wafuatao:

   i. Washiriki wa Wizara, Idara na Taasisi za Serikali;

   ii. Uwakilishi wa Taasisi za Elimu za Serikali na binafsi;

iii. Uwakilishi wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa yanayojishughulisha na masuala ya watoto;

iv. Uwakilishi wa mashirika ya kimataifa yanayojishughulisha na masuala ya watoto;

v. Uwakilishi wa Asasi za Kiraia wanaoshughulika na masuala ya watoto;

vi. Uwakilishi wa Taasisi za Dini;

vii. Uwakilishi wa Sekta Binafsi;

viii. Uwakilishi wa Mataifa mbalimbali;

ix. Uwakilishi wa Mabalozi wanaowakilisha Nchi zao nchini Tanzania;

x. Uwakilishi wa watu wenye ulemavu;

xi. Wadau mbalimbali wa MMMAM;

xii. Uwakilishi wa Vyombo Habari; na

xiii. Uwakilishi wa wazazi na watoto

2.1.3.1 Sekretarieti ya PJT-MMMAM Ngazi ya Taifa

Idara ya Maendeleo ya Mtoto ndiye Mwenyekiti wa Sekretarieti ya PJT-MMMAM. Idara ya Ustawi wa Jamii ni Makamu Mwenyekiti.

Sekretarieti ya programu ya MMMAM itaundwa na wajumbe wafuatao:

i. Uwakilishi wa Wizara zinazotekeleza PJT-MMMAM.

ii. Uwakilishi wa Mashirika ya Umoja wa Mataifa.

iii. Uwakilishi wa Mashirika ya Kimataifa yanayotekeleza PJT-MMMAM.

iv. Uwakilishi wa Asasi za Kiraia zinazotekeleza PJT-MMMAM

v. Mtandao wa Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (TECDEN)

Vikao vya Sekretarieti ya PJT-MMMAM Ngazi ya Taifa

a) Sekretarieti ya PJT-MMMAM itakutana mara moja kwa mwezi na kutakuwa na vikao vya dharura pale itakapohitajika.

b) Akidi ya wajumbe wa kikao cha Sekretarieti ya PJT-MMMAM itakuwa zaidi ya nusu ya wajumbe akiwemo mwenyekiti .

c) Wajumbe wa sekretarieti wanapaswa kushiriki katika kuandaa na kutekeleza majukumu ya kiutawala na mawasiliano wakati na baada ya vikao.

Majukumu ya Sekretarieti ya uratibu wa PJT-MMMAM ngazi ya Taifa

a) Kuandaa vikao na mikutano yote ya kikanuni ya Mawaziri, Makatibu Wakuu, Kamati Tendaji ya MMMAM na Jukwaa la wadau wa MMMAM

b) Kuchukua na kutunza kumbukumbu za mikutano yote ya kikanuni na wadau wa PJT-MMMAM;

c) Kufuatilia utekelezaji wa maazimio ya vikao vya kikanuni vya Mawaziri, Makatibu Wakuu, Kamati Tendaji ya MMMAM na Jukwaa la wadau wa MMMAM

d) Kufuatilia, kutathmini, na kutoa taarifa ya utekelezaji na kushauri utekelezaji wa PJT-MMMAM

e) Kusaidia utafutaji wa rasilimali kwa ajili ya uratibu

f) Kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa PJT-MMMAM.

g) Kushawishi ujumuishaji wa ajenda za Malezi Jumuishi katika vikao vya kitaalamu vya kisekta;

h) Kupendekeza maeneo ya tafiti za MMMAM na Kuainisha tafiti zinazohusiana na PJT-MMMAM ili kupata matokeo ya utafiti yatakayosaidia katika upangaji wa mipango ya MMMAM;

i) Kubadilishana uzoefu kuhusiana na mbinu zilizoleta matokeo chanya katika utekelezaji wa PJT-MMMAM.

2.1.4 Wizara yenye dhamana na Afya

Wizara yenye dhamana na Afya itahakikisha vipengele vya MMMAM vinajumuishwa kwenye Sera, Mikakati, Programu, Kanuni na Miongozo na kutenga rasilimali kwa ajili kutekeleza afua mahususi za MMMAM katika sekta ya afya.

Majukumu ya Wizara yenye dhamana na Afya

a) Kuratibu utoaji wa huduma bora za MMMAM katika sekta ya Afya

b) Kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa PJT-MMMAM kwenye vikao vya uratibu ngazi ya Taifa

c) Kujenga uelewa wa PJT-MMMAM ndani ya Wizara na taasisi zake

d) Kushirikiana na Taasisi zilizo chini ya Wizara kuratibu masuala ya afya na lishe kupitia OR-TAMISEMI

e) Kushirikiana na Wizara za Kisekta na Wadau katika utekelezaji wa PJT-MMMAM

f) Kujumuisha masuala ya MMMAM kwenye tafiti za Afya na Lishe.

2.1.5 Wizara yenye dhamana na Elimu

Wizara yenye dhamana na Elimu itahakikisha vipengele vya MMMAM vinajumuishwa kwenye Sera, Mikakati, Programu, Kanuni na Miongozo na kutenga rasilimali kwa ajili kutekeleza afua mahususi za MMMAM katika sekta ya elimu.

Majukumu ya Wizara yenye dhamana na Elimu

a) Kuratibu utoaji wa huduma bora za MMMAM katika sekta ya elimu
b) Kushirikiana na Taasisi zilizo chini ya Wizara katika kutekeleza PJT-MMMAM
c) Kushirikiana na Wizara za Kisekta na Wadau katika utekelezaji wa PJT-MMMAM
d) Kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa PJT-MMMAM kwenye vikao vya uratibu ngazi ya Taifa
e) Kujenga uelewa wa PJT-MMMAM ndani ya Wizara na taasisi zake
f) Kujumuisha masuala ya MMMAM kwenye tafiti za elimu

2.1.6 Wizara yenye dhamana na Mambo ya Ndani ya Nchi

Wizara yenye dhamana na Mambo ya Ndani ya Nchi itahakikisha vipengele vya MMMAM vinajumuishwa kwenye Sera, Mikakati, Programu, Kanuni na Miongozo; na kutenga rasilimali za kutosha kwa ajili kutekeleza afua mahsusi za MMMAM katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi

Majukumu ya Wizara yenye dhamana na Mambo ya Ndani ya Nchi

a) Kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa PJT-MMMAM kwenye vikao vya uratibu ngazi ya Taifa
b) Kushirikiana na Wizara za Kisekta na Wadau katika utekelezaji wa PJT-MMMAM
c) Kujenga uelewa wa PJT-MMMAM ndani ya Wizara na taasisi zake

2.1.7 Wizara yenye dhamana na Fedha

Wizara yenye dhamana na Fedha itahakikisha vipengele vya MMMAM vinajumuishwa kwenye Sera, Mikakati, Kanuni na Miongozo na kutenga rasilimali kwa ajili kutekeleza afua mahsusi za MMMAM nchini.

Majukumu ya Wizara yenye dhamana na Fedha

a) Kuingiza masuala ya MMMAM katika miongozo ya uandaaji wa mipango na bajeti za kila mwaka.
b) Kubainisha kiasi cha fedha kilichotengwa katika uwekezaji wa masuala ya MMMAM.
c) Kushirikiana na Wizara za Kisekta na Wadau katika utekelezaji wa PJT-MMMAM

2.1.8 Wizara yenye dhamana na Watu wenye Ulemavu

Wizara yenye dhamana na Watu wenye Ulemavu itahakikisha vipengele vya MMMAM vinajumuishwa kwenye Sera, Mikakati, Kanuni na Miongozo na kutenga rasilimali za kutosha kwa ajili kutekeleza afua mahsusi za MMMAM nchini.

Majukumu ya Wizara yenye dhamana na Watu wenye Ulemavu

a) Kujumuisha masuala ya MMMAM kwenye sera, miongozo na programu zinazohusu watu wenye ulemavu
b) Kuwasilisha taarifa ya utekelezaji wa PJT-MMMAM kwenye vikao vya uratibu ngazi ya Taifa
c) Kushirikiana na Wizara za Kisekta na Wadau katika utekelezaji wa PJT-MMMAM

2.1.9 Ngazi ya Mkoa

Katika ngazi ya Mkoa uratibu wa PJT-MMMAM utakuwa chini ya Afisa Ustawi wa Jamii Mkoa. Mratibu atafanya kazi kwa kushirikiana na wataalamu wengine wa MMMAM ikiwa ni pamoja na; Afisa Maendeleo ya Jamii Mkoa, Afisa Lishe wa Mkoa, Mratibu wa Mama na Mtoto, Katibu Tawala Msaidizi Elimu, Katibu Tawala Msaidizi Mipango na Uratibu na Katibu Tawala Msaidizi Afya. Kikao cha Kamati ya Ushauri ya Mkoa kitapokea na kujadili masuala ya MMMAM. Wasimamizi wa shughuli za MMMAM wakishirikiana na Mratibu wa PJT-MMMAM ngazi ya Mkoa wataandaa taarifa na kuiwasilisha katika kamati ya ushauri ya Mkoa.

Majukumu ya mratibu wa PJT-MMMAM ngazi ya mkoa

a) Kukusanya taarifa za utekelezaji wa MMMAM kutoka sekta husika na kuandaa taarifa kwa ajili ya kuwasilisha kwenye kamati ya ushauri ya Mkoa.

b) Kufuatilia utekelezaji wa maazimio ya Kamati ya Ushauri ya Mkoa kuhusu MMMAM.

c) Kufuatilia, kutathmini, na kutoa taarifa ya utekelezaji kila robo mwaka na kushauri utekelezaji wa PJT-MMMAM

d) Kusaidia utafutaji wa rasilimali kwa ajili ya uratibu

e) Kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa PJT-MMMAM

f) Kushawishi ujumuishaji wa ajenda za Malezi Jumuishi katika vikao vya kitaalamu vya kisekta

g) Kubadilishana uzoefu kuhusiana na mbinu zilizoleta matokeo chanya katika utekelezaji wa PJT-MMMAM.

h) Kuandaa kikao cha tathmini ya utekelezaji wa programu ngazi ya Mkoa.

i) Kujengea uwezo watekelezaji wa PJT-MMMAM.

j) Kufanya usimamizi shirikishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuona utekelezaji wa programu.

k) Kuwabaini na kuwaratibu wadau waliopo ngazi ya Mkoa wanaotekeleza PJT-MMMAM

l) Kufanya uchambuzi wa mipango na bajeti za Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa

2.1.10 Ngazi ya Wilaya

Katika ngazi ya Wilaya kila Halmashauri itakuwa na Mratibu wa PJT-MMMAM ambaye atakuwa Afisa Ustawi wa Jamii. Mratibu atafanya kazi kwa kushirikiana na wataalamu wengine wa MMMAM ikiwa ni pamoja na; Afisa Maendeleo ya Jamii, Afisa Lishe, Mratibu wa Mama na Mtoto, Afisa ELimu, Afisa Mipango na Uratibu na Mganga Mkuu. Kikao cha kamati ya Ushauri ya Wilaya kitapokea na kujadili masuala ya MMMAM kutoka Mamlaka za Serikali za Mtaa.

Katika Mamlaka za Serikali za Mitaa masuala ya MMMAM yatawasilishwa katika vikao vya Kamati za kudumu (Elimu, Afya na Maji; Uchumi na Mazingira; na Fedha, Uongozi na Mipango), Kamati ya Wataalam ya Halmashauri (*Council Management Team*) na Baraza la Madiwani

Majukumu ya mratibu wa PJT-MMMAM ngazi ya Halmashauri

a) Kukusanya taarifa za utekelezaji wa MMMAM kutoka sekta husika na kuandaa taarifa kwa ajili ya kuwasilisha kwenye kamati ya ushauri ya Wilaya.

b) Kuandaa na kuwasilisha taarifa ya PJT-MMMAM kwenye Kamati za kudumu (Elimu, Afya na Maji; Uchumi na Mazingira; na Fedha , Uongozi na Mipango), Kamati ya Wataalam ya Halmashauri (Council Management Team) na Baraza la Madiwani

c) Kufuatilia utekelezaji wa maazimio ya Kamati ya Ushauri ya Wilaya kuhusu MMMAM.

d) Kufuatilia utekelezaji wa maazimio ya Kamati za kudumu (Elimu, Afya na Maji; Uchumi na Mazingira; na Fedha , Uongozi na

Mipango), Kamati ya Wataalam ya Halmashauri (Council Management Team) na Baraza la Madiwani

e) Kufuatilia, kutathmini, na kutoa taarifa ya utekelezaji kila robo mwaka na kushauri utekelezaji wa PJT-MMMAM

f) Kusaidia utafutaji wa rasilimali kwa ajili ya uratibu

g) Kuhamasisha ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa PJT-MMMAM

h) Kushawishi ujumuishaji wa ajenda za Malezi Jumuishi katika vikao vya kitaalamu vya kisekta

i) Kubadilishana uzoefu kuhusiana na mbinu zilizoleta matokeo chanya katika utekelezaji wa PJT-MMMAM.

j) Kujengea uwezo watekelezaji wa PJT-MMMAM.

k) Kufanya usimamizi shirikishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kuona utekelezaji wa programu.

l) Kuwabaini na kuwaratibu wadau waliopo ngazi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa wanaotekeleza PJT-MMMAM

m) Kufanya uchambuzi wa mipango na bajeti za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kushirikiana na wasimamizi wa MMMAM ili kuona namna ambavyo afua za MMMAM zimezingatiwa

2.1.11 Ngazi ya Kata

Uratibu wa PJT-MMMAM ngazi ya Kata:

Uratibu ya PJT-MMMAM ngazi ya Kata utakuwa chini ya Afisa Ustawi wa Jamii. Taarifa ya masuala ya MMMAM katika ngazi ya Kata itawasilishwa katika Kamati ya Maendeleo ya Kata. Endapo afisa aliyetajwa kuratibu PJT-MMMAM hatakuwepo Mkurugenzi wa Halmashauri atateua mratibu ngazi ya Kata kadri anavyoona inafaa.

Majukumu Mratibu wa PJT-MMMAM ngazi ya Kata:

a) Kuandaa taarifa ya utekelezaji wa PJT-MMMAM na kuiwasilisha kwenye kikao cha Kamati ya Maendeleo ya Kata

b) Kusimamia utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto katika kata.

c) Kupokea na kujadili taaarifa ya utekelezaji wa programu kutoka katika ngazi ya kijiji/Mtaa.

d) Kuhamasisha Utekelezaji wa Programu katika Kata.

e) Kufuatilia na kutathmini Utekelezaji wa Programu katika Kata.

f) Kujenga uwezo wa watekelezaji wa Programu katika Kata

g) Kubaini na kuratibu wadau wote wanaotekeleza PJT-MMMAM katika Kata

2.1.12 Ngazi ya Kijiji/Mtaa

Uratibu wa PJT-MMMAM ngazi ya Kijiji/Mtaa:

Uratibu ya PJT-MMMAM katika Kijiji/Mitaa utakuwa chini ya Mtendaji wa Kijiji/Mtaa Taarifa ya masuala ya MMMAM katika Kijiji/Mtaa itawasilishwa katika Halmashauri ya Kijiji/Mtaa.

Majukumu ya Mratibu wa PJT-MMMAM ngazi ya Kijiji/Mtaa:

a) Kuandaa taarifa ya utekelezaji wa PJT-MMMAM na kuiwasilisha kwenye Halmashauri ya Kijiji/Mtaa

b) Kusimamia utekelezaji wa Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi, Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto katika Kijiji/Mtaa.

c) Kuhamasisha Utekelezaji wa Programu katika Kijiji/Mtaa.

d) Kufuatilia na kutathmini Utekelezaji wa Programu katika Kijiji/Mtaa.

e) Kujenga uwezo wa watekelezaji wa Programu katika Kijiji/Mtaa

f) Kubaini na kuratibu wadau wote wanaotekeleza PJT-MMMAM katika Kijiji/Mtaa

3.0 UFUATILIAJI, TATHMINI NA UTOAJI TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA PJT- MMMAM

3.1 Ufuatiliaji na tathmini

Ufuatiliaji katika utekelezaji wa PJT-MMMAM utahusisha ukusanyaji na uchambuzi wa taarifa ambazo zitatumika kubaini masuala yaliyochochea mafanikio na changamoto kwenye kila ngazi ya utekelezaji. Tathmini itazingatia utekelezaji wa kila jukumu lililoainishwa kwenye ngazi husika na kufuatilia rasilimali watu na fedha zilizotengwa na zilizotumika katika utekelezaji wa programu.

Tathmini ya kati ya utekelezaji wa Programu kitaifa itafanyika katika mwaka wa fedha 2023/24 na tathmini ya mwisho itafanyika mwaka 2025/26. Aidha, kutakuwa na vipindi mbalimbali vya kufanya tathmini ambavyo ni kila robo mwaka kwa ngazi ya Halmashauri, kata na Kijiji / Mtaa, nusu mwaka kwa ngazi ya Mkoa na kila mwaka kwa ngazi ya Taifa.

Ufuatiliaji na tathmini utafanyika kwa kuzingatia maeneo mbalimbali ikiwa ni pamoja na:

i. Uratibu wa sekta mbalimbali kwenye ngazi zote katika utekelezaji wa PJT-MMMAM;

ii. Uzingatiaji wa Sera, Sheria na Miongozo iliyopo katika Utekelezaji wa PJT-MMMAM;

iii. Uwepo wa watoa huduma wenye ujuzi na umahiri katika maeneo ya MMMAM;

iv. Uwepo wa mfumo wa ufuatiliaji, tathmini na ujifunzaji uliokubalika kwa ajili ya PJT-MMMAM;

v. Uwepo wa taarifa zenye takwimu ili kuboresha utekelezaji wa PJT-MMMAM;

vi. Upatikanaji wa huduma za MMMAM katika jamii;

vii. Utengaji na Utumiaji wa rasilimali kwa ajili ya utekelezaji wa PJT-MMMAM; na

viii. Ushiriki wa Wadau mbalimbali katika utekelezaji wa PJT-MMMAM.

3.2 Utoaji Taarifa ya Utekelezaji wa PJT-MMMAM

Ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa PJT-MMMAM utaambatana na utoaji wa taarifa ya utekelezaji kupitia mifumo na vikao mbalimbali vya kikanuni pamoja na vikao maalum kuanzia ngazi ya Kijiji/ Mtaa, Kata, Halmashauri, Mkoa na Taifa.

4.0 HITIMISHO

Utekelezaji wa mwongozo wa uratibu wa PJT-MMMAM utatengeza mazingira wezeshi na kuboresha juhudi za kufikia matokeo ya programu ambayo ni:

- Mazingira wezeshi yameboresha kuwezesha uratibu wenye ufanisi na utoaji wa huduma za malezi jumuishi.
- Mifumo ya utoaji huduma jumuishi za MMMAM na uthibiti ubora imeimarishwa;
- Kuongezeka kwa upatikanaji wa huduma bora na zilizoratibiwa za malezi jumuishi kwa watoto wenye umri wa miaka 0-8 na walezi wao; na
- Wazazi, walezi, familia na jamii wamejengewa uwezo wa kutekeleza taratibu sahihi za Malezi jumuishi.

Ni muhimu juhudi zifanyike kila wakati kujenga uwezo wa rasilimali watu katika ngazi mbalimbali kuhakikisha waratibu, watekelezaji na wafuatiliaji wa afua za PJT- MMMAM wanakuwa na ufanisi katika ngazi zote. Katika kufikia malengo inashauriwa kutumia mfumo jumuishi katika kuhakikisha upatikanaji wa rasilimali, utekelezaji wa shughuli na matokeo yenye tija kwa wakati.

Pamoja na kuwa taarifa na takwimu kuhusiana na afua za MMMAM zinaweza kuhitajika kupitia mifumo, ni muhimu taarifa hizo zitunzwe kupitia mifumo iliyopo ambayo inaendana na PJT-MMMAM. Mifumo hii ambayo inatajwa katika PJT- MMMAM ni pamoja na mifumo ya takwimu za Kitaifa, za kisekta ikiwemo ya afya, elimu, lishe, Ustawi, Maendeleo ya Jamii, Ulinzi na Usalama.

Ikumbukwe kuwa utekelezaji wa Mwongozo huu haujengi mfumo mpya bali unatumia mifumo iliyopo ya uratibu ikiwemo Kamati za Uratibu na Miundo ya Utawala na Uongozi katika ngazi husika ili kuhakikisha huduma za MMMAM zinahuishwa na kuwa endelevu. Halikadhalika, matumizi ya mifumo hii yataepusha kudurufu miundo ya utekelezaji na ufuatiliaji wa afua zinazohusu Watoto.

Mchoro Na. 1: Uratibu wa Programu Jumuishi ya Taifa ya MMMAM, Ufuatiliaji na tathmini na muundo wautekelezaji



Mwongozo wa Uratibu wa Programu Jumuishi ya Taifa ya Malezi Makuzi na Maendeleo ya Awali ya Mtoto (PJT-MMMAM) 2021/22–2025/26